

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

*Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA*  
*Simu Na.:* (026) 2333848, 2321607  
2322853, 2322420  
*Nukushi:* (026) 2322116, 2322146  
2321013  
*Barua pepe:* [ps@tamiseemi.go.tz](mailto:ps@tamiseemi.go.tz)



*Tawala za Mikoa  
na Serikali za Mitaa,  
(TAMISEMI),  
Mji wa Serikali - Mtumba,  
S.L.P. 1923,  
DODOMA.*

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUJAZA NAFASI ZA WALIMU  
NA WALIMU WA AJIRA MBADALA AMBAO HAWAKURIPOTI  
KWENYE VITUO MWEZI APRILI-MEI, 2019**

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapenda kuutarifu Umma kuwa, jumla ya Watumishi **116** wamepangiwa vituo vya kazi kwenye Shule mbalimbali za Msingi na Sekondari nchini. Watumishi wanajaza nafasi wazi za watumishi ambao hawakuripoti kwenye vituo waliopangiwa mwezi Aprili, 2019. Waajiriwa hao waliopangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuripoti katika Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zilipo shule walizopangiwa na baadaye kuripoti kwenye Shule walizopangiwa kuanzia **tarehe 12 hadi 26 Julai, 2019** wakiwa na mahitaji yafuatayo:

- (i) Vyeti halisi vya taaluma vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita;
- (ii) Vyeti halisi vya kitaalam vya Mafunzo ya Ualimu vya ngazi husika; na
- (iii) Cheti halisi cha kuzaliwa.

Waajiriwa wapya waliopangiwa vituo vya kazi wanaelekezwa kuwa:

- i. Waajiriwa wote waripoti kwenye vituo walivyopangiwa na kwamba vituo vyao vya kazi ni katika Shule za Sekondari walizopangiwa na sio Makao Makuu ya Halmashauri;

- ii. Mwajiriwa ye yote atakayechukua posho ya kujikimu, kisha asiripoti katika kituo chake cha kazi alichopangiwa, Serikali atamchukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za nchi;
- iii. Hakuna Mwajiriwa atakayebadilishiwa kituo alichopangiwa kwa sababu yoyote ile.

Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo Watumishi hao wamepangiwa, wawapokee kwa kuzingatia taratibu na kanuni zote za utumishi na baadaye kutoa taarifa ya kuripoti kwa walimu hao. Taarifa ya Waajiriwa hao zitumwe OR-TAMISEMI mara baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti.

Majina ya Walimu waliopangiwa vituo vya kazi yanapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI ya [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz).

11/07/2019

Imetolewa na  
KATIBU MKUU